**HOTUBA YA MWL. JULIUS KAMBARAGE NYERERE WAKATI WA KUZALIWA CHAMA CHA MAPINDUZI MWAKA 1977**

Waheshimiwa Wakuu wa Nchi, Waheshimiwa Mabalozi na wageni wetu wengine, Waheshimiwa marafiki zetu wote na ndugu wananchi;

Chama cha TANU kilipoanzishwa hatukufanya sherehe, Chama cha *African Association* na *Shirazi Association* vilipoungana na kuunda Chama kimoja *Afro Shirazi Party* hapakuwa na sikukuu yoyote, lakini leo siku ya kuanzisha Chama Cha Mapinduzi tumethubutu kupiga mbiu. Tumekaribisha Wajumbe kutoka vyama vingine vingi vya kijamaa na tumewapokea wageni kutoka nchi nyingi za kirafiki. Kwa kitendo hiki tumejishtaki wenyewe hadharani. Kama TANU ingeshindwa kutimiza shabaha zake za kuleta Uhuru lisingekuwa jambo la aibu kwa wale waliokutana kimya kimya Mjini Dar es Salam na kuunda chama chenye shabaha hiyo. Kama ASP ingegawanyika au ingeruhusu hila na mbinu za Sultani zivunje nguvu zake waanzilishi wa chama hicho wasingeweza kusutwa kwa kujigamba kwao.

Katika vyama vyote hivyo viwili, wale walioshiriki kuviunda walikuwa wamejitolea nafsi zao kufanya kazi ngumu na ya kihistoria. Kama wangeshindwa, kazi hiyo hiyo ingeweza kushikwa na watu wengine na vyama vingine, waanzilishi wa TANU na waanzilishi wa ASP wangepata heshima yao ya kujaribu na wengine wangejifunza kutokana na ujuzi wao na vilevile kutokana na makosa yao, lakini sisi tunathubutu kutangaza

kuundwa kwa Chama cha Mapinduzi na kusherehekea kitendo hicho kuwa ni kitendo cha mafanikio.

Vilevile kila Mtanzania ambaye leo anajitangaza kuwa mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi anatangaza ahadi yake ya kuwa mwaminifu kwa chama na kufanya juhudi  kukisaidia Chama Cha Mapinduzi kutimiza shabaha zake, maana tunatangaza shabaha hizi kwa watu wote duniani na wakati huo huo tunajitangaza hadharani kwamba sisi ndiyo Chama Cha Mapinduzi na kwamba Chama Cha Mapinduzi ndiyo sisi. Tumethubutu kuyafanya hayo na tuna haki ya kuthubutu. Muungano wa TANU na ASP ni muungano wa vyama vikubwa viwili vyenye uwezo na mafanikio.

Kila kimoja kilikuwa chama chenye mamlaka ya mwisho katika eneo lake, kila kimoja kilikuwa kinatambua kazi yake iliyobaki, kila kimoja kilipendwa na kuaminiwa na maelfu ya wanachama wake baada ya kuvitumikia kwa muda wote huo wa miaka 20 au hata zaidi. Vyama vyote viwili TANU na ASP vilikuwa ni vyama vyenye uhai na vyama vyenye uwezo, maelfu ya wanachama walijitolea kuvitumikia maisha yao yote na wengine walikuwa wakivifanyia kazi ama za kuchaguliwa au za kuteuliwa na sasa hawana hakika kama wataendelea na kazi hizo baada ya kuunganisha vyama vyetu*.* Kwa hiyo, kujitolea kwa hiyari kwa Vyama vya TANU na ASP kukipisha chama kipya ni ushindi wa msimamo wa kimapinduzi katika mapambano yake na msimamo wa ubinafsi na upinga mapinduzi. Ni ushahidi wa vitendo vya watu wanaoshikilia msingi wa huduma, haitoshi kusema daima, lakini kwa maneno matupu kwamba umoja ni nguvu, lazima tuthibitishe kwa

vitendo vyetu kwamba tunaamini kweli kuwa umoja ni nguvu. Kinapotendwa kitendo cha kimapinduzi kama hicho, wanaokitenda wana haki ya kukitangaza na wana haki ya kukisherehekea. Kuanzishwa kwa Chama Cha Mapinduzi ni dalili ya dhahiri inayoonesha kuwa watu wa Tanzania wamekusudia kwa dhati kutimiza shabaha yao ya kujenga nguvu za kijamaa. Shabaha hiyo ina maana zaidi kwetu sisi na kwa vizazi vyetu kuliko chama chochote hata kama chama hicho kimefanya kazi kubwa huko nyuma. Hatuwezi kuishi kwa kutazama nyuma, lazima tuishi kwa kutazama mbele tunakokwenda.

Kwa hiyo, fikra njema za TANU na ASP sasa zimehamishiwa katika chombo kikubwa zaidi kuliko TANU na kuliko ASP peke yake na chombo ambacho kitatufaa zaidi katika mahitaji yetu ya siku za mbele. Kuanzishwa kwa Chama Cha Mapinduzi ni kitendo cha watu waliodhamiria kuleta mapinduzi katika maisha yao kwa utaratibu mzuri na kwa njia ya uamuzi wa makusudi wa wananchi wenyewe. Chama Cha Mapinduzi kimeanzishwa kwa uamuzi wa ki-*demokrasi* na Chama cha Mapinduzi kitakuwa ni chama cha ki-*demokrasi* kazi zake ni ngumu, zitahitaji moyo na kujitolea kwa wanachama na rafiki zake kila siku. TANU iliwaongoza wananchi wa Tanzania Bara kufikia Uhuru kwa njia ya siasa na kufikia lengo la kuleta ujamaa; ASP iliwaongoza wananchi wa Tanzania Visiwani kupata Uhuru kwa njia ya siasa pia, lakini hatima yake wakalazimika kufanya mapinduzi.

Kazi hizi zilikuwa ngumu, zilizohitaji moyo na wakati mwingine zilikuwa kazi za kutisha, lakini vilevile zilikuwa kazi za kusisimua, maana mkoloni alikuwa

ni adui wa nje na alikuwa ni adui anayeonekana. Lazima Chama Cha Mapinduzi kiendelee kupambana na ukoloni mamboleo kazi ambayo TANU na ASP ilikuwa imekwisha kuianza, lakini pia lazima Chama Cha Mapinduzi kiwaongoze wananchi wa Tanzania katika kazi ngumu zaidi kuliko hiyo iliyotangulia, mapambano ya kuleta uhuru wa ndani ya Tanzania, uhuru wa kila mwananchi binafsi, siyo uhuru wa nchi tu kama huu tuliokwisha kuupata. Chama chetu kipya kinapaswa kuongoza katika juhudi za maendeleo ya uchumi na haki za uchumi na za uhuru wa kweli wa kila binadamu, ndani ya misingi ya nchi ambayo imani yake ni usawa, heshima na ushirikiano wa binadamu wote. Hakuna jambo lolote katika mapambano yetu ya siku za nyuma ambalo ni gumu kama kazi hii ambayo tumetangaza hadharani kuwa tunaianza.

TANU na ASP vimeweka msingi, vyama hivi viwili vimeleta uhuru wa kisiasa katika Jamhuri yetu ya Muungano, vimenyakua uchumi wa nchi yetu kutoka katika mikono ya mabepari ambao walikuwa wakitunyonya kutoka humu nchini na vimeweka vyombo ambavyo ni vya lazima kwa kujengea nchi ya kijamaa na nchi ya ki-demokrasi, lakini kazi yenyewe ya kujenga ujamaa haijaisha, hii ni kazi ya Chama Cha Mapinduzi, maana ujamaa sio suala la utaratibu tu au la kuweka vyombo vya umma peke yake. Ujamaa pia ni tabia na vitendo, ujamaa ni uhusiano wa mtu na mtu na mtu na umma, ni usawa na utu, ni kuheshimu na kuheshimiana, ni haki na ni wajibu na mambo haya hayapatikani kwa amri wala kwa sheria, yatakuzwa tu kwa uongozi bora na mifano mizuri ya maadili ya kijamaa. Kwa hiyo, demokrasi katika mambo ya siasa na ya uchumi ni sehemu ya ujamaa.

Hatutajaribu kujenga ujamaa bila demokrasi na wala hatujajaribu kujenga demokrasi bila ujamaa, hatujui maana ya kimoja bila kingine, lakini vyombo na utaratibu wa ki-demokrasi peke yake havitoshi na wala vyombo na utaratibu wa kijamaa peke yake havitoshi, lazima vyombo hivyo vitumiwe na wananchi na ili vitumiwe lazima wananchi waelewe haki zao na wajibu wao, lazima wajiamini wao wenyewe na wawe na imani na madaraka yao.

Ndugu wananchi ukweli ni kwamba tabia zetu zinatokana na historia yetu chini ya ubepari na ukoloni na mila zetu za zamani, urithi wetu sio wa ki-demokrasi na wala sio wa kijamaa. Mtoto aliyezaliwa katika Tanzania huru ndiye aliyeanza kidogo kidogo kulelewa katika mazingira ya ki-demokrasi na ya kijamaa, lakini kijana huyo bado hajatimiza umri wa kudai haki na kutimiza wajibu alionao Mtanzania mtu mzima na wala malezi hayo ya ki-demokrasi na kijamaa ambayo tumeyaanza bado hayajakamilika. Fikra tulizorithi za mabwana na watwana, matajiri na maskini, bado zingali akilini mwetu na mara nyingi sana zinasababisha vitendo vyetu viende kinyume cha msimamo wetu.  Tumekuja na fikra hizo katika kazi ya kujenga nchi ya kijamaa na ya kidemokrasi  ambamo tunataka watu wote wawe na haki na heshima sawa, nchi ambamo hakuna mtu anayeishi kwa anasa wakati watu wengine bado wana dhiki, nchi ambamo mtu hamuonei mtu mwingine.

Wananchi tunaanza upya, Chama Cha Mapinduzi ni Chama kinachoanzishwa mwaka 1977. Shabaha zake na madhumuni yake ingawa ni yale yale ya zamani yanatangazwa upya mwaka 1977. Sisi wanachama wake na viongozi wake ni wale wale na kasumba zetu ni zile zile, lakini

tunaahidi upya kwamba tutajitahidi kwa uwezo wetu wote kuzifuta kasumba hizo kutoka vichwani mwetu, lakini ingawa chama ni sisi, chama chenyewe hakina kasumba.

Chama chetu hakianzi na tabaka za watoaji amri na wapokeaji amri, msingi wa chama chetu kipya ni kukataa tabaka na kukataa madaraka yanayotumiwa kwa faida za mtu binafsi. TANU na ASP vimejenga vyombo vyetu vya ujamaa na demokrasi. Kazi ya Chama Cha Mapinduzi si kujenga tena vyombo zaidi vya ujamaa na demokrasi kazi ya Chama Cha Mapinduzi ni kuviimarisha vyombo hivyo na kuvitumia kwa ufanisi zaidi kutekeleza kazi yake.

Chama Cha Mapinduzi hakina budi kisimamie vizuri maendeleo ya uchumi wetu, Chama Cha Mapinduzi hakina budi kisimamie vizuri zaidi vyombo vyetu vya siasa, Chama Cha Mapinduzi hakina budi kihakikishe kwamba vyombo hivyo vinalindwa na haviachwi na vikashambuliwa na vibaraka wa ubepari na ukoloni mamboleo. Kazi ya Chama Cha Mapinduzi ni kuwaongoza Watanzania kulinda uhuru wao na heshima ya nchi yao. Kazi ya Chama Cha Mapinduzi ni kuwaongoza Watanzania wajenge ujamaa nchini mwao. Kazi ya Chama Cha Mapinduzi ni kuwaongoza Watanzania washirikiane na Waafrika wenzao kuleta uhuru na umoja katika Afrika nzima.

Kazi ya Chama Cha Mapinduzi ni kuwaongoza Watanzania washirikiane na binadamu wenzao kuleta haki na amani duniani; Chama Cha Mapinduzi ni

Chama cha watu; Chama Cha Mapinduzi kitaongoza kutoka miongoni mwa watu na kitaongoza kikiwa ni sehemu ya Watanzania maana wananchi ndio waliokiunda Chama Cha Mapinduzi kiwe chombo chao na kiongozi wao. Sisi ambao leo tunajitangaza hadharani kuwa wanachama wa Chama Cha Mapinduzi tunajitolea maisha yetu kwa huduma hiyo, tunafanya hivyo tukiwa watu miongoni mwa watu, tunafanya hivyo tukiwa watu sawasawa na wale waliotuamini kutupa madaraka hayo au ambao tunajua kwamba wanaweza kutunyima nafasi hiyo kama wakiona kuwa hatuzistahili.

Tumwombe Mwenyezi Mungu basi, atuwezeshe kukitumia chombo hicho ambacho tumekiunda leo ili kitekeleze mahitaji ya wananchi wa Tanzania na wananchi wa Bara letu la Afrika kwa mujibu wa fikra zao na kwa faida ya maendeleo yao. Tumwombe Mwenyezi Mungu atusadie tuepukane na vishawishi vya matumizi mabaya ya madaraka na uwezo ambao Chama Cha Mapinduzi kitakuwa kinao ili siku zote vitendo vyetu viwe ni vitendo vya maadili ya kijamaa katika nchi yenye heshima, haki na usawa kwa watu wote.

Kwa mara nyingine tena, nawashukuru wageni wetu wote kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa pamoja nasi katika sherehe hizi za siku hii ambayo kwetu ni siku ya kumbukumbu.  Ahsanteni sana.